#WeweNdoFuture #TimizaWajibu

# HESLB Yako

Jarida la Mtandaoni la Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu | Toleo No. 4
Octoba - Desemba 2021

# TZS 570 BILIONI ZATOLEWA MIKOPO ELIMU YA JUU

Na Mwandishi Wetu
Dar es salaam

Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) hadi kufikia Desemba 31, 2021 imelipa kiasi cha TZS 529 Bilioni kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu iliyonufaisha jumla ya wanafunzi 176,617 kwa mwaka wa masomo 2021/2022.

Aidha kiasi cha TZS 41 Bilioni pia zimepangwa kulipwa kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya mafunzo kwa vitendo, na hivyo kufanya fedha zote zilizotolewa na Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Samia Suluhu Hassan kufikia kiasi cha TZS 570 Bilioni. Akizungumza na HESLB Yako, Mkurugenzi Msaidizi Upangaji Mikopo HESLB, Deus Changala alisema mikopo hiyo imetolewa kwa wanafunzi wa makundi mbalimbali ambao waliwasilisha maombi yao ya mikopo katika mwaka wa masomo 2021/2022.

Changala alisema kwa upande wa wanafunzi wa mwaka wa kwanza, hadi kufikia Desemba 31 mwaka 2021, HESLB ilikuwa imeshawapangia mikopo kwa wanafunzi wa mwaka wa kwanza 69,274 yenye thamani ya TZS 178.7 Bilioni.

"Kwa mwaka 2021/2022, Serikali ilipanga kutoa mikopo kwa wanafunzi 70,000 wa mwaka wa kwanza na hadi sasa tayari tumeweza kuwapangia mikopo wanafunzi 69,274, idadi hii ni kubwa ukilinganisha naidadi ya wanafunzi 55,387 tuliowapangia mikopo kwa mwaka 2020/2021" amesema Changala.

Aidha Changala alisema HESLB pia imepanga mikopo kwa wanafunzi 107,343 wanaoendelea na masomo yenye thamani ya TZS 350.2 Bilioni na kusisitiza kuwa malengo ya Serikali ni kuhakikisha kuwa fedha zote zinalipwa kwa wakati ili wanafunzi wasome kwa utulivu.

Kwa mujibu wa Changala makundi mengine ya wanafunzi waliopangiwa mikopo ni pamoja na wanaosoma nje ya nchi, ambapo kiasi cha TZS 759 Milioni kimetolewa na Serikali kwa ajili ya kusomesha wanafunzi 99 waliopo katika nchi mbalimbali duniani.

Alizitaja nchi hizo kuwa ni Algeria, Msumbiji, Urusi na China na kuongeza kuwa HESLB imekuwa ikitoa sehemu ya fedha kama mikopo ama ruzuku kwa niaba ya serikali kwa nyakati tofauti kwa wanafunzi wanaosoma katika baadhi ya nchi wahisani na marafiki wa Tanzania.

Akifafanua zaidi Changala alisema HESLB pia imelipa kiasi cha kiasi TZS 636 Milioni kwa wanafunzi 120 wanaoendelea na masomo ya shahada za uzamili na uzamivu katika vyuo mbalimbali nchini na kuendelea kuzitaka menejimenti za vyuo vikuu nchini kuhakikisha kuwa malipo yote ya fedha za mikopo ya wanafunzi zinalipwa kwa wakati.



## NDANI...



05 HUSNA: HESLB IMETIMIZA NDOTO ZANGU

08 RITA: YAHAKIKI VYETI 524,619 - 2017-2021



09 MUSTSO: USHIRIKIANO NA MENEJIMENTI...

10 TPC KUBORESHA VITUO 322 MIKOPO ELIMU YA JUU



## JAMBO LETU



Ismail Ngayonga
*Mhariri*

# KOMAENI NA NDOTO & MALENG0 ACHANENI NA 'BATA'

Tarehe 15 Oktoba mwaka huu, Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu ilianza kutangaza orodha ya awamu ya kwanza ya Wanafunzi wa mwaka wa kwanza waliopangiwa mikopo kwa mwaka wa masomo 2021/2022.

Hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2021 HESLB ilikuwa imepanga mikopo kwa wanafunzi 176,617 yenye thamani ya TZS TZS 529 Bilioni wakiwemo wanafunzi 69,274 wa mwaka wa kwanza na wanafunzi 107,343 wanaoendelea na masomo.

Fedha zote zilizotolewa na HESLB tayari zimetumwa vyuoni kwa ajili ya kukamilisha taratibu za malipo kwa wanafunzi hao, hivyo ni wajibu wa Menejimenti za Vyuo kuhakikisha Maafisa Mikopo wanaharakisha malipo ya fedha hizo ili kulipwa kwa wakati mara baada ya wanafunzi kukamilisha taratibu zote za usajili.

Ni vyema kwa wanafunzi wahitaji kutambua kuwa, HESLB imekamilisha wajibu wake wa kutoa fedha za mikopo na hivyo ni wajibu wao kusoma kwa bidii na kuhakikisha kuwa malengo na dhamira ya Serikali ya kutenga fedha za bajeti yanatimia katika kuzalisha wataalamu wa kada mbalimbali nchini. Tunatoa rai kwa viongozi wa Serikali za wanafunzi vyuoni kuendelea kushirikiana na menejimenti za vyuo katika kutatua na kushughulikia changamoto zinazoweza kujitokeza na kuziwasilisha katika madawati husika ili kupatiwa ufumbuzi.

HESLB inawaahidi viongozi wa Serikali za wanafunzi na menejimenti za vyuo kuwa itaendeleza mashirikiano yaliyopo ili kuvifanya vyuo vikuu na taasisi za elimu ya juu kuendelea kuwa na mazingira bora ya kutoa elimu kwa vijana wa Kitanzania katika kutimiza malengo na shahaba zilizowekwa na Serikali.

Menejimenti ya HESLB inawatakia heri ya wanafunzi wote waliojiunga na vyuo na taasisi za elimu na wale wanaoendelea na masomo na kuhakikisha wanasoma kwa bidii kwa kutambua Serikali itaendelea kuwawezesha kupata mikopo kwa wakati katika kipindi chote cha masomo yao vyuoni.

BODI YA UHARIRI

**Mwenyekiti**
Abdul-Razaq Badru

**Katibu**
Omega Ngole

**Wajumbe**
Veneranda F. Malima
Ismail Ngayonga
Eline Maronga
Jonathan Nkwabi
Jacqueline Msuya

**Designer**
+255 736 190 083

**Mawasiliano**
Mkurugenzi Mtendaji
Bodi ya Mikopo ya
Wanafunzi wa Elimu ya Juu
1 Mtaa wa Kilimo, TAZARA
S.L.P 76068
Dar es salaam
Tanzania

**WhatsApp:** 0736 665 533
**Barua Pepe:** adcp@heslb.go.tz
**Tovuti:** heslb.go.tz

HESLB
BODI YA MIKOPO
INVESTING IN THE FUTURE



"Tarehe 3 Desemba mwaka huu, HESLB ilibuka mshindi wa tatu kwa taasisi za umma zinazotumia mwongozo wa "IPSAS" katika uandaaji wa hesabu kwa mwaka 2020 katika tuzo iliyokabidhiwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA).

# TUTAENDELEZA UFANISI WA HUDUMA ZETU

Ndugu wasomaji wetu karibuni katika Toleo No. 3 la Jarida la HESLB Yako ambalo huchapishwa kupitia njia ya mtandao likiwa ni moja ya kiungo cha mawasiliano baina yetu na wadau wetu.

Tarehe 3 Desemba mwaka huu, HESLB ilibuka mshindi wa tatu kwa taasisi za umma zinazotumia mwongozo wa "IPSAS" katika uandaaji wa hesabu kwa mwaka 2020 katika tuzo iliyokabidhiwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA).

Tuzo hiyo ambayo ni matokeo ya shindano lililoshirikisha jumla ya taasisi 71 kutoka sekta binafsi na umma, katika kundi lililoishirikisha HESLB, mshindi wa kwanza ilikuwa ni Mamlaka ya Mapato Tanzania na mshindi wa pili ni Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC).

Halikadhalika mafanikio yaliyopo ni kutokana na maboresho ya mifumo ya Teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) kuanzia hatua ya wanufaika kuomba mikopo, kuchambua na kutoa fedha za mikopo kwa walengwa.

Katika kipindi cha miaka minne mfululizo (2016-2020), HESLB imeendelea kupata hati safi¬ kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Hii ni ishara tosha kuwa fedha zinatolewa na Serikali kwa ajili ya mikopo ya wanafunzi zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Aidha kuimarika kwa mifumo kumeiwezesha HESLB kujiunga na mfumo wa serikali wa malipo ya kieletroniki (GePG). Kwa kupitia GePG, wadau husussan wanufaika na waajiri wanaendelea kuelewa wajibu wao wa kuhakikisha fedha za mikopo ya wanufaika zinakatwa na kuwasilishwa HESLB kwa wakati kama Sheria inavyoelekeza.

Tumejipanga kuhakikisha kuwa mwaka 2022 Menejimenti na watumishi wote wa HESLB tunaongeza ubunifu na maarifa katika kujituma na kuhakikisha tunaendelea kufanya kazi kwa weledi ili kuweza kufikia malengo ya kitaasisi.

KUTOKA KAMPAS



# HESLB IMECHAGIZA SAFARI YANGU UDSM

**Na Mwandishi Wetu**

Dar es salaam

NI mpole, mkimya, msikivu na mwenye shauku ya kubuni na kuvumbua mambo mapya katika siku za Usoni. Huyu ni Hyasinta Luhanga (22), mtakwimu na mwanahisabati wa Shahada ya Sayansi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) mwaka wa tatu.

Hyasinta anaielezea HESLB Yako safari yake ya elimu ya juu ilivyojaa furaha kutokana na mkopo wa elimu ya juu aliopatiwa na HESLB na jinsi ulivyomwezesha kuishi katika ndoto ya matumaini ya kuitumikia jamii ya Watanzania katika siku za usoni.

"Naishukuru HESLB kwa kunipatia mkopo wa elimu ya juu kwa asilimia 100, isingekuwa rahisi kwa kipato cha mama yangu mzazi ambaye ndiye aliyekuwa na jukumu la kunisomesha masomo yangu ya "O-Level" hadi "A-Level" baada ya baba yangu mzazi kufariki mwaka 2012," anasema Hyasinta.

Aidha Hyasinta anaeleza kuwa familia yao ina jumla ya watoto 2 akiwemo yeye na kaka yake ambaye aliishia masomo ya Stashahada, hivyo yeye alijitahidi kusoma kwa bidii ili kuhakikisha anafikia ndoto za kusoma masomo ya chuo kikuu ili aweze kuitumikia jamii inayomzunguka.

Anaeleza kuwa mara baada ya kuhitimu masomo yake ya kidato cha sita katika Shule ya Sekondari Tambaza mwaka 2019 na kupata ufaulu wa daraja la kwanza katika masomo ya mchepuo wa Sayansi (Fizikia, Kemia na Hisabati) alipata taarifa za masuala ya mikopo ya elimu ya juu kutoka HESLB.

Kwa mujibu wa Hyasinta, mara baada ya kupata taarifa hizo kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii, alitembelea tovuti ya HESLB www.heslb.go.tz na kusoma mwongozo wa uombaji mikopo ulioainisha sifa, vigezo na taratibu za uombaji mikopo kwa wanafunzi wahitaji.

"Nilisoma kwa umakini mkubwa mwongozo uliotolewa na HESLB kwani nilitambua kuwa huo ndio ufunguo wa maisha yangu ya baadae. Baada ya kukamilisha taratibu zote za maombi. Naishukuru HESLB ilinipangia mkopo wangu kwa 100%", alisema Hyasinta.

Akifafanua zaidi, Hyasinta alipongeza juhudi za Serikali katika kuongeza bajeti za mikopo ya elimu ya juu mwaka hadi mwaka na kwamba hicho ni kielelezo cha dhamira ya serikali katika kusomesha Watanzania wahitaji katika ngazi ya elimu ya juu.

"Katika mwaka huu wa masomo 2021/2022, kimetengwa kiasi cha TZS 570 Bilioni. Hiki ni kiasi kikubwa cha fedha ambacho serikali imezielekeza katika elimu ya juu. Nawasihi wanafunzi wenzangu tuzitumie fedha hizi katika malengo yaliyokusudiwa", amesema Hyasinta.

# HYASINTA



**Desemba 3, 2021;** Mhasibu Mkuu wa HESLB, Brown Shimwela akionesha tuzo ya ushindi wa nafasi ya tatu kwa taasisi za umma katika uandaaji wa hesabu kwa mwaka 2020 kwa kutumia mwongozo "IPSAS" iliyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA) wakati wa hafla iliyofanyika Jijini Dar es Salaam.



**Novemba 15, 2021:** Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru akitoa ufafanuzi kwa wajumbe wa kamati ya Ustawi ya Jamii ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar wakati walipofanya ziara katika Ofisi za HESLB, Jijini Dar es Salaam.



**Novemba 16, 2021;** Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknojia, Prof. Joyce Ndalichako (waliokaa katikati) akiwa katika picha ya pamoja na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo wakati wakati wa ufunguzi wa kikao kazi cha Maafisa Habari, Elimu na Mawasiliano wa Wakala na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo Mkoani Morogoro.



**Novemba 23, 2021;** Meneja wa HESLB, Ofisi ya Mtwara Rukia Semwaiko akitoa ufafanuzi wa majukumu ya HESLB kwa Mkuu wa Mkoa wa Mtwara, Brigedia Jenerali Marco Gaguti wakati alipotembelea Banda la HESLB katika Shamrashamra za maadhimisho ya miaka 60 ya uhuru Mkoani humo.



**Oktoba 11, 2021:** Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Mhandisi Robert Gabriel (kushoto) akimkabidhi tuzo ngao ya ushindi, Afisa Mikopo wa Chuo Kikuu Kishirikishi cha Elimu Dar es Salaam (DUCE), Daudi Salmon wakati wa Kikao kazi cha Maafisa Mikopo kilichofanyika tarehe 11-12 Oktoba,2021 Jijini Mwanza. Katikati ni Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru.

# Husna

## HESLB imetimiza ndoto zangu

**Na Mwandishi Wetu**
Mtwara

NDOTO huzaa tafsiri ya malengo katika maisha ya binadamu. Simulizi ya Mwanafunzi Husna Mbewe (26) wa Chuo cha Stella Marris Mtwara (STEMMUCO) ina mafunzo na mazingatio ndani yake.

Husna, mwanafunzi wa mwaka wa kwanza Shahada ya Sanaa (Sociology) anasema hakuna kipingamizi cha yeye kufikia ndoto ya kuwa Afisa Maendeleo ya Ustawi wa Jamii, baada ya kupata mkopo wa elimu ya juu kutoka HESLB.

Anasema mkopo wa elimu ya juu umemwezesha kupata uhakika wa kufikia malengo yake katika kuwatetea na kuwasaidia watu wa jamii ya walemavu nchini ili waweze kupata huduma na haki mbalimbali za msingi.

"Mimi ni mlemavu wa ngozi, naishukuru HESLB kwa kuniwezesha kupata mkopo wa elimu ya juu. Nimepanga kuwa Afisa Ustawi wa Jamii ili niweze kuielimisha jamii inayonizunguka pale Kijijini kwetu Liwale B na Tanzania kwa ujumla na kuhakikisha inakombolewa," anasema Husna. Husna anasema anaishukuru Ofisi ya HESLB Mtwara kwa kumpatia usaidizi wakati wa kukamilisha fomu za maombi ya mkopo, ambapo Maofisa walifika Chuoni hapo kwa ajili ya kutoa elimu kwa waombaji mikopo na yeye akiwa ni miongoni mwa washiriki wa semina hiyo.

Anaongeza kuwa kabla ya mchakato wa maombi ya mkopo alihakikisha anasoma mwongozo na kuandaa nyaraka muhimu ambazo ni pamoja na vyeti vya kuzaliwa vilivyohakikiwa na RITA na barua ya Mganga Mkuu yenye kuthibitisha hali ya ulemavu aliyonayo. "Nashukuru nimepangiwa vipengele vyote vya mkopo ikiwemo ada ya masomo, vitabu na viandikwa, chakula na malazi n.k. Tunamshukuru sana Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kwani kwa hali ya wazazi wangu ambao ni wakulima, wasingeweza kunisomesha masomo ya chuo kikuu", anasema Husna.

Husna Mbewe ni mtoto wa pili na ndiye pekee alifanikiwa kufika elimu ya chuo kikuu kati ya watoto nane (8) wa Bw. Hashim Mbewe (46) na Bi. Maimuma Chilumba (42), ambao ni wakulima katika Kijiji cha Liwale B, Wilaya ya Liwale Mkoani Lindi.



> Mimi ni mlemavu wa ngozi, naishukuru HESLB kwa kuniwezesha kupata mkopo wa elimu ya juu. Nimepanga kuwa Afisa Ustawi wa Jamii ili niweze kuielimisha jamii inayonizunguka pale Kijijini kwetu Liwale B na Tanzania kwa ujumla na kuhakikisha inakombolewa
>
> **Anasema Husna.**




# MSOVU

## KUREJESHA MKOPO WA ELIMU NI UZALENDO

**Na Mwandishi Wetu**
Dar es salaam

> Serikali ilifanya jambo jema kuanzisha chombo hiki. Kwa hali ya uwezo wa kiuchumi wa familia yangu nisingeweza kusoma elimu ya juu. Naishukuru HESLB kwa kunipatia mkopo kwa asilimia 100, sasa mimi ni msomi najivunia kulitumikia taifa langu

Waswahili wanasema "Uungwana ni vitendo na" Hii ni kauli ya Mnufaika wa HESLB, Haji Msovu (39) ambaye kwa sasa ni Afisa Uhusiano wa Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Jijini Dodoma.

Msovu, ni Msomi wa Shahada ya Mawasiliano ya Umma kutoka Chuo Kikuu cha Waislamu Morogoro (2005-2008) na anazungumza na Mwandishi wa HESLB Yako kuhusu Simulizi ya historia yake ya elimu na maisha.

Hivi karibuni, Msovu alimaliza kulipa deni la Mkopo wa elimu ya juu la kiasi cha TZS 6,289, 625/- aliopatiwa na HESLB na anaeleza simulizi, ushuhuda na nasaha kwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu kuhusu umuhimu wa urejeshaji wa mikopo hiyo.

Anasema baada ya kumaliza masomo ya shahada ya kwanza mwaka 2008 na kupata ajira katika Shule ya Sekondari Fredrick Sumaye iliyopo Wilaya ya Babati, Mkoani Manyara, aliamua kufika katika ofisi za HESLB, Msasani, Jijini Dar es Salaam ili kupata utaratibu wa kurejesha mkopo wake.

Akifafanua zaidi Msovu anasema ni hali ya uzalendo iliyomsukuma kurejesha mkopo, na hii ilitokana na kutambua wajibu wake kama mnufaika kwani malengo ya Serikali kuanzisha HESLB ni kuwa na Mfuko endelevu unaowezesha kusomesha wanafunzi Watanzania wahitaji.

"Serikali ilifanya jambo jema kuanzisha chombo hiki. Kwa hali ya uwezo wa kiuchumi wa familia yangu nisingeweza kusoma elimu ya juu, naishukuru HESLB kwa kunipatia mkopo kwa asilimia 100, sasa ni msomi najivunia kulitumikia taifa langu," alisema Msovu.

Kwa mujibu wa Msovu, wakati alipoanza kurejesha mkopo wa elimu ya juu mwaka 2008 alianza na makato ya kiasi cha TZS 38,000 na ambapo hata hivyo ilipofika mwaka 2009 kiwango hicho kiliongeza na kufikia TZS 56,000/- hatua iliyotokana na kubadilishwa kwa kada ya utumishi.

"Nilianzia utumishi wangu katika kada ya ualimu na baadaye mwaka 2012 nilihama kada na kuwa Afisa Habari katika Halmashauri ya Mji Babati, mshahara ulibadilika na makato nayo yaliongezeka, haikunisumbua sana katika kurejesha kwani tayari ndoto yangu ya kufika chuo kikuu ndani ya familia yetu niliitimiza," anasema Msovu.

Anaongeza kuwa alitumia muda wa miaka saba kumaliza kulipa deni la elimu ya juu, na alipomaliza alifanya mawasiliano na Ofisi ya HESLB na mwezi Julai mwaka huu alipatiwa barua ya kumaliza kulipa mkopo wa HESLB.

Aidha Msovu alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kufuta tozo ya ongezeko la thamani ya mkopo (VRF) kwani imeleta unafuu na ahueni kwa wanufaika na hivyo kuwasihi wanufaika wote ambao mikopo yao imeiva kujitokeza na kurejesha ili kuweza kuwasomesha wanafunzi wahitaji.

"Tunamshukuru Mhe. Rais kwa maelekezo yake kwa HESLB kufuta tozo za VRF na adhabu ya 10% ya mikopo. Hii itaongeza hamasa zaidi kwa wanufaika kuweza kurejesha mikopo yao. Nawasihi wanufaika waendelee kujitokeza ili kuifanya HESLB kuwa na mfuko endelevu na kusomesha wanafunzi wengi zaidi," alisema Msovu.

# MILAMBO MALEGI

## MWL. MZALENDO ALIVYOSIFURISHA DENI LAKE

**Na Mwandishi Wetu**
Mwanza



Dhana ya Uzalendo ni falsafa inayoendelea kuhimizwa na viongozi na watendaji wa serikali na dini katika maslahi ya ujenzi wa taifa. Kwa Milambo Malegi (47) ambaye ni mnufaika wa mikopo ya elimu ya juu kutoka HESLB, amezaliwa na tunu ya uzalendo na kuwa na moyo wa kujitolea kwa manufaa ya wengi, kama anavyoeleza katika simulizi yake na Mwandishi wa HESLB Yako.

"Nilihitimu masomo yangu ya Shahada ya Ualimu katika Chuo cha SAUT mwaka 2009, nikiwa ni miongoni mwa wanufaika wa mikopo ya elimu ya juu, ambapo nililipiwa na HESLB kuanzia mwaka 2006-2009," anaeleza Milambo Malegi, Mwalimu wa masomo ya Kiswahili na Jiografia.

Mwalimu Malegi anasema wakati alipojiunga na masomo ya Shahada ya Uzamili katika Chuo cha SAUT mwaka 2015, aliguswa na hali ya uhitaji wa mkopo wa Serikali kwa wanafunzi wa shahada ya kwanza chuoni hapo na ndipo Desemba mwaka 2016 alifika ofisi za HESLB Mwanza kupata taarifa ya deni lake na kuanza marejesho ya mkopo huo.

"Wakati naanza kurejesha, nilianza na marejesho ya kiasi cha TZS 150,000/- na baadae mwezi Agosti, 2021 niliongeza kiasi cha makato na kufikia TZS 250,000. Nashukuru mwezi Oktoba mwaka huu, nimefanikiwa kumaliza deni langu", anasema Mwalimu Malegi.

Mwalimu Malegi anasema baada ya tamko la Mhe. Rais mwezi Mei, mwaka huu, alifika katika Ofisi za HESLB na kupata ufafanuzi na taarifa za hali ya mkopo wake ambapo alikuta mkopo wa deni lake umepungua kutoka TZS 7,752,000 hadi TZS 952,347.64, na kuamua kulipa kiasi kilichobaki ili kumaliza deni lake.

Akifafanua zaidi Mwalimu Malegi anasema anajisikia fahari na kupata faraja kubwa kumaliza mkopo wa elimu ya juu, na hivyo kutoa hamasa kwa wanufaika wengine kujitokeza ili kuanza kurejesha kwani sasa mkopo huo umekuwa himilivu kutokana na ahueni na nafuu iliyotolewa na Serikali wakati wa kurejesha.

Anasema kwa sasa amekuwa Balozi wa HESLB katika Mikoa ya Kanda ya Ziwa kwani kwa kushirikiana na Ofisi ya HESLB Kanda ya Ziwa, amekuwa akishiriki katika kuandaa vipindi maalum vya redio kwa ajili ya kuelimisha wanufaika ili wajitokeze kwa hiari na kurejesha mikopo yao.

Mwalimu Malegi anawasihi wanufaika wengine kuwa na moyo wa uzalendo na kujitolea kwa ajili ya maendeleo ya taifa kwa kutambua kuwa vijana ni taifa la kesho linalohitaji msaada mkubwa kutoka kwao katika kurejesha mikopo ya elimu ya juu.



# RITA

## YAHAKIKI VYETI 524,619 VYA WAOMBAJI MIKOPO - 2017-2021

**Na Mwandishi Wetu**
Dar es Salaam

Wakala wa Usajili, Udhamini na Ufilisi (RITA) imehakiki jumla ya vyeti vya waombaji mikopo ya wanafunzi wa elimu ya juu 524,619 katika kipindi cha miaka mitano (2017-2021) kupitia mfumo wa E-Huduma.

Akizungumza na HESLB Yako, Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu wa RITA, Emmy Hudson amesema katika kipindi cha miaka mitano sasa, RITA imepiga hatua kubwa katika matumizi ya Tehama kwa ajili ya kuhakiki Vyeti vya wanafunzi, ambapo kwa sasa mwombaji hutuma nyaraka na kupokea majibu kwa njia ya kielektroniki.

"Huduma za uhakiki hutolewa kwa njia ya Mtandao tu kupitia mfumo wa E-Huduma ambapo mwombaji anaweza kutuma maombi ya kupata cheti au uhakiki akiwa nyumbani na hata ikiwa ni kijijini na pia mfumo huo ni rafiki na rahisi kutumia", alisema Emmy.

Emmy alisema uhakiki wa Nyaraka ni moja ya jukumu la RITA na hufanyika kwa lengo la kubaini uhalali wa vyeti kutokana na kuibuka kwa wimbi la watu wasio waaminifu wanaoghushi nyaraka kwa lengo la kujipatia huduma mbalimbali za serikali ikiwemo uombaji mikopo ya elimu ya juu.

Aidha, Emmy alisema katika kutekeleza Mpango wa Usajili wa watoto wa umri kati ya miaka 5-17, ambao ni wanafunzi katika shule za msingi na sekondari, RITA imewawezesha wanafunzi wa shule za msingi na sekondari zaidi ya 512,207 kupata vyeti vya kuzaliwa na hivyo kupunguza idadi ya wanafunzi wanaotaka kuomba mikopo ya elimu ya juu ambao hawana vyeti vya kuzaliwa.

Kuhusu mipango ya baadae ya taasisi hiyo, Emmy alisema RITA inaendelea kuboresha upatikanaji wa huduma zake kupitia Mkakati wa Kitaifa wa Usajili wa Matukio Muhimu ya Binadamu na Takwimu kwa kusogeza huduma karibu na makazi ya wananchi, pamoja na matumizi ya TEHAMA katika kutuma taarifa na maombi.

# MUSTSO

## TUNAPONGEZA USHIRIKIANO NA HESLB, MENEJIMENTI

**Na Mwandishi Wetu**
Mbeya

JUMUIYA ya Serikali ya Wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUSTSO), imepongeza ushirikiano inayoendelea kupatiwa na Menejimenti ya Chuo na HESLB katika kushughulikia changamoto za wanafunzi.

Rais wa MUSTSO, Amani Mdekha anaieleza HESLB Yako kuwa kutokana na ushirikiano uliopo, Chuo hicho kimeweza kutatua changamoto mbalimbali za wanafunzi ikiwemo suala la mikopo ya wanafunzi, ambapo zaidi ya 62% ya wanafunzi wa shahada ya kwanza wameweza kupangiwa mikopo.

"MUST ina wanafunzi 4,000 wanaosoma shahada ya kwanza katika kozi mbalimbali. Tunapongeza na kushukuru juhudi za Serikali za kuendelea kutuongezea idadi ya wanufaika wa mikopo mwaka hadi mwaka. Hii imetokana na ushiriakiano mzuri baina ya Menejimenti ya MUST na Serikali ya Wanafunzi" alisema Mdekha.

Kwa mujibu wa Mdekha, ongezeko hilo la wanufaika limewezesha pia kuongezeka kwa idadi ya wasomi nchini na hivyo kusaidia kupatikana kwa wataalam wa kada mbalimbali watakaosaidia taifa kupiga hatua kimaendeleo.

Akizungumzia kuhusu bajeti ya mikopo ya mwaka 2021/2022, Mdekha alisema Serikali imekuwa ikifanya juhudi kubwa katika kuboresha sekta ya elimu ya juu nchini kuanzishwa kwa HESLB kumewezesha kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanufaika wa mikopo wa elimu ya juu mwaka hadi mwaka.

"Fedha za mikopo kwa sasa zinawafikia wanafunzi kwa wakati ukilinganisha na kipinidi cha nyuma ambapo jambo hili lilipelekea kuwa na migomo mingi vyuoni. Kwa sasa HESLB pamoja na serikali zimejitahidi kuhakikisha wanafunzi tunazipata fedha hizi kwa wakati kupitia mfumo wa DiDiS," anasema Mdekha.

Aidha Mdekha alipongeza juhudi zilizofanywa na Rais Samia Suluhu Hassan za kufuta tozo na adhabu mbalimbali za mikopo ya wanafunzi, kwani hatua hiyo itaongeza hamasa kwa wanufaika wengi zaidi kujitokeza na kuanza kurejesha mikopo yao.

"Napenda kuwakumbusha wanafunzi wenzangu kuwa fedha hizi ni mikopo, hivyo tunapaswa kuzirejesha mara tunapohitimu masomo yetu, na tunapaswa kutambua kuwa nyuma yetu kuna ndugu na jamaa zetu ambao nao watakuja kusoma elimu ya juu, hivyo tukumbuke kurejesha fedha za mikopo" alisema Mdekha.



# TPC YATENGA TZS 3.9 BILIONI KUBORESHA VITUO 322 MIKOPO ELIMU YA JUU




**Na Mwandishi Wetu**
Dar es Salaam

Shirika la Posta Tanzania (TPC) limetenga TZS 3.9 Bilioni ili kuongeza ufanisi wa Shirika hilo katika utumaji, usafirishaji na uwasilishwaji wa barua zikiwemo fomu za maombi ya mikopo ya wanafunzi katika mwaka 2021/2022.

Akizungumza katika mahojiano maalum na HESLB Yako, Kaimu Meneja Mkuu Uendeshaji Biashara TPC, Constantine Kasese alisema maboresho hayo ni kufuatia mabadiliko ya Sayansi na Teknolojia, ambapo TPC imedhamiria kuwekeza zaidi katika mifumo ya TEHAMA katika uendeshaji wa shirika hilo kibiashara.

"Kwa zaidi ya miaka 10 sasa, TPC imeendelea kuhudumia wanafunzi katika uombaji wa mkopo ya elimu ya juu ambao wamekuwa wadau wakubwa sana. Tumeboresha miundombinu muhimu ikiwemo Maboresho katika mifumo na vituo vya huduma ya mtandao (Internet Café) ", alisema Kasese.

Halikadhalika, Kasese aliongeza katika kuwezesha maombi ya mikopo ya wanafunzi kupitia mpango huo wa Maboresho. TPC imejikita katika kuimarisha vituo vyake vyote kwa kuviwezesha kwa vitendea kazi ambavyo ni kompyuta, magari makubwa na madogo na pikipiki za magurudumu mitatu.

Kwa mujibu wa Kasese, TPC linapongeza ushirikiano kati ya HESLB na TPC uliodumu kwa zaidi ya miaka 10 sasa, na kwamba mabadiliko mbalimbali yaliyokuwa yamefanyika yamesaidia kuziimarisha taasisi zote mbili na kuchochea ongezeko la mapato.

"HESLB wana kampeni ya WeweNdoFuture inayomlenga mwombaji Mkopo kuwa ndiye atakayeweza kupata elimu na kuisaidia Taifa letu na kusisitiza kurejesha mkopo huo pindi anapohitimu masomo. Kwetu sisi TPC kampeni hii inatupa hamasa katika kuongeza ubora na ufanisi wa huduma zetu", alisema Kasese.

# SALUTI

## MHE RAIS SAMIA SULUHU HASSAN

Na Mwandishi Wetu
Morogoro



WASWAHILI wanasema "baada ya dhiki, faraja", Kauli hii inathibitishwa na ukweli wa historia ya mnufaika wa mikopo ya Elimu ya Juu, Magreth Mwanjala mwaka wa kwanza, Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) Mkoani Morogoro.

"Ni safari ndefu kutoka Kijiji cha Ifisi, Wilaya ya Mbeya hadi kufika hapa SUA. Naishukuru sana Serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuniwezesha kupata mkopo wa elimu ya juu uliotimiza malengo yangu," anaanza kusimulia.

Magreth ni miongoni mwa wanafunzi 70,000 waliopangiwa mikopo kwa mwaka 2021/2022 na anasema anatamani kuonana ana kwa ana na Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kutoa shukrani za moja kwa moja kwake kutokana na HESLB kumpangia mkopo wa elimu ya juu.

"Sisi ni watoto yatima tulipoteza wazazi wetu wote wawili. Nilipata faraja zaidi nilipopangiwa mkopo wa elimu ya juu na HESLB. Namshukuru Rais Samia ameonesha kwa kitendo kuwa yeye ni Mama halisi, amerejesha faraja katika familia yetu", amesema Magreth.

Aidha, Magreth alisema wakati wa mchakato wa maombi ya mikopo alihakikisha anakamilisha taratibu zote ikiwemo kuweka vyeti vya vifo vya wazazi wake na kujaza fomu kwa usahihi, na hivyo kuwaasa wanafunzi wenye sifa na uhitaji wa mikopo kusoma mwongozo ili kuweza kujaza fomu za maombi kwa usahihi.

"Binafsi nawasihi wahitaji wenye sifa kujaza fomu kwa usahihi. Mikopo ya elimu ya juu inatolewa kwa wanafunzi wote na haina upendeleo. Jambo muhimu ni kusoma mwongozo wa uombaji mikopo, kujaza fomu kwa usahihi na kutuma maombi kwa wakati", alisema Magreth.

Magreth ambaye ni mwanafunzi wa mwaka wa kwanza SUA katika Shahada ya Usimamizi wa Utalii (BTM) anasema alipenda kusoma kozi hiyo kutokana na ukweli kuwa alivutiwa na masuala ya utalii hususan eneo la uhifadhi na usimamizi wa wanyamapori.

> Binafsi nawasihi wahitaji wenye sifa kujaza fomu kwa usahihi. Mikopo ya elimu ya juu inatolewa kwa wanafunzi wote na haina upendeleo. Jambo muhimu ni kusoma mwongozo wa uombaji mikopo, kujaza fomu kwa usahihi na kutuma maombi kwa wakati
>
> **Alisema Magreth.**

# HESLB YAONGOZA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TUZO ZA NBAA 2020

**Na Mwandishi Wetu**
Dar es Salaam

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imeibuka mshindi wa tatu kwa taasisi za umma zinazotumia mwongozo wa viwango vya kimataifa wa hesabu za umma (International Public Sector Accounting Standards) "IPSAS" katika uandaaji wa hesabu kwa mwaka 2020 katika tuzo zinazoratibiwa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu (NBAA).

Tuzo hiyo ilikabidhiwa Desemba 3, 2021 kwa HESLB na Mhasibu Mkuu wa Serikali, (CPA) Leonard Mkude, ambapo katika kundi hilo mshindi wa kwanza ilikuwa ni Mamlaka ya Mapato Tanzania na mshindi wa pili Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC).

Tuzo hizo ziligawanywa katika makundi 13 ya kisekta, ambapo HESLB ilishuhudia kwa upande wa taasisi za elimu ya juu; Taasisi ya Ustawi wa Jamii (ISW) na Chuo Kikuu cha Kikristo cha Afya Bugando (CUHAS) pia zikiibuka washindi katika shindano hilo lililoshirikisha jumla ya taasisi 71 kutoka sekta binafsi na umma.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi ya NBAA, Prof. Slyvia Temu alisema upatikanaji wa washindi wa tuzo ulifanyika kwa kuzingatia vigezo vya wazi na vya kitaaluma ikiwemo kuwa na hati safi na kuwasilisha hesabu kwa wakati na pia kufikisha kiwango cha ubora wa taarifa.

Kwa upande wake, CPA (T) Leonard Mkude ambaye alimwakilisha Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha na Mipango, Bw. Emmanuel Tutuba, alizipongeza taasisi zilizojitokeza kushiriki katika shindano hilo kwa vile linalenga kuongeza ufanisi.

"Kwa taasisi zote zilizoshiriki, natoa wito zipokee maoni na matokeo ya ushiriki kwa maoni chanya na kuboresha", amesema Mkude.

Akizungumzia tuzo hiyo baada ya kuipokea, Mhasibu Mkuu wa HESLB CPA (T) Brown Shimwela alisema wameipokea kama chachu ya kuongeza ufanisi zaidi.

"Tuzo hii ni matokeo ya uboreshaji wa mifumo ya fedha, mikopo, taarifa za wateja wetu na ushirikiano wa wafanyakazi wote….tutaendelea kuboresha ufanisi", amesema Shimwela. Mashindano hayo yalianzishwa na NBAA miaka 10 iliyopita na HESLB ilianza kushiriki mwaka 2018/2019 ambapo ilishika nafasi ya nne (04) kwa taasisi za Serikali zinazoandaa hesabu kwa mwongozo wa "IPSAS".



Desemba 3, 2021; Mhasibu Mkuu wa HESLB, Brown Shimwela akionesha tuzo ya ushindi wa nafasi kwa taasisi za umma katika uandaaji wa hesabu kwa mwaka 2020 kwa kutumia mwongozo "IPSAS" iliyotolewa na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi (NBAA) wakati wa hafla iliyofanyika Jijini Dar es Salaam.


## OFISI ZETU

**DAR ES SALAAM**
HESLB HOUSE, 1 KILIMO STREET,
TAZARA AREA, MANDELA ROAD,
P.O BOX 76068, 15471 DAR ES SALAAM
INFO@HESLB.GO.TZ

**DODOMA**
JENGO LA PSSSF, BR. YA MAKOLE,
KITALU 4&5, BLOCK W. ENEO LA UHINDINI,
SIMU: 0758 067 577 | 0739 067 577
DODOMA@HESLB.GO.TZ

**ZANZIBAR**
JENGO LA ZSTC, KINAZINI, BR. MALAWI,
S.L.P 900, ZANZIBAR,
SIMU: 0779 321 424
ZANZIBAR@HESLB.GO.TZ

**ARUSHA**
NSSF JENGO LA MAFAO, GROROFA YA KWANZA,
S.L.P 2712, ARUSHA,
SIMU: 027 2520128 | 0624 100011 | 0739 102016
ARUSHA@HESLB.GO.TZ

**MWANZA**
PSSSF PLAZA, GROROFA YA PILI,
FRONT WING, BR. KENYATTA, S.L.P 3051, MWANZA,
SIMU: 028 2506008 | 0759 819350 | 0738 153661
MWANZA@HESLB.GO.TZ

**MBEYA**
JENGO LA CAG, BR. MBALIZI,
S.L.P 319, MBEYA,
SIMU: 0738 131310 | 0738 131311
MBEYA@HESLB.GO.TZ

**MTWARA**
NHC RAHA LEO COMPLEX GROROFA YA PILI
KIWANJA NA. 217 KITALU H,
KARIBU NA OFISI YA MKUU WA MKOA
S.L.P 969, MTWARA, SIMU: 0736 026 668
MTWARA@HESLB.GO.TZ

HESLB Tanzania HESLB_Tanzania

#WeweNdoFuture
#TimizaWajibu